

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**17 MEI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 17 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 243. MHESHIMIWA BRYCESON MAGESSA TUMAINI (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali italipatia Jimbo la Busanda Vituo vya Afya hususan Tarafa za Butundu na Busanda.

#### 244. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za Wananchi katika ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya Kata za Arumeru Mashariki.

#### 245. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuongeza bajeti ya TARURA Wilayani Ngorongoro ili kukabiliana na uharibifu wa barabara uliotokana na mvua kubwa zilizonyesha msimu wa Mwaka 2019/2020.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**246. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

- (a) Je, Serikali imejipanga vipi kupambana na tishio la uvuvi haramu nchini;
- (b) Je, ni Meli ngapi zilikamatwa nchini tangu Mwaka 2015 – 2020 kwa kosa la uvuvi haramu.

**WIZARA YA MAJI:**

**247. MHESHIMIWA KUNTI YUSSUF MAJALA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto kubwa ya maji inayowakabili Wananchi wa Mji wa Chemba.

**248. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO  
(BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mabwawa makubwa ambayo yatahifadhi maji ya mvua ili yaweze kutumika kwa shughuli za Kibinadamu, Kilimo na Mifugo katika Mkoa wa Dodoma ambao umekuwa haupati mvua za kutosha.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**249. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI  
(KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na Waganga wapiga ramli chonganishi na Manabii wa uongo wanaodanganya na kutapeli Wananchi kila siku.

**250. MHESHIMIWA JANETH ELIAS  
MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya huduma za Kipolisi katika maeneo ya pembezoni mwa Miji ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**251. MHESHIMIWA AUGUSTINE VUMA HOLLE (KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Kasulu - Uvinza kwa kiwango cha lami.

**252. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Wananchi wa Idofi watalipwa fidia baada ya maeneo yao kuchukuliwa na Serikali kwa ajili ya kujenga Mradi wa Idofi *One Stop Centre*.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA**  
**17 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**